# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 20 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Oktoba 2023

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


# MATUMIZI YA MBOLEA KULETA TIJA KWENYE KILIMO - DKT. SAMIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan akifungua mjadala wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu usalama wa chakula na juhudi zinazofanywa na nchi hizo kuhakikisha uzalishaji wa chakula unaongezeka wakati wa mkutano wa Jukwaa la Chakula Afrika ambapo zaidi ya watu 4000 kutoka nchi mbalimbali wameshiriki.


NDANI>>

Ruzuku ya mbolea ina ukomo: Rais Dkt. Samia 4

Utegemezi wa mbolea nje ya Afrika wapelekea matumizi hafifu, uzalishaji mdogo 6

Naibu Waziri Silinde aitaka TFRA kuimarisha Udhibiti wa Mbolea 8




# Matumizi ya mbolea kuleta tija kwenye kilimo - Dkt. Samia




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mjadala maalum wa vijana uliofnyika katika Ukumbi wa Selous katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere tarehe 7 Septemba, 2023

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alieleza kuwa,ongezeko la kiasi cha mbolea inayotumika kwenye shughuli za kilimo ni ishara tosha kuwa kilimo kinaleta tija kwa wakulima.

Alisema, kuongezeka kwa uzalishaji kwenye miradi mbalimbali ya kilimo inayosimamiwa na vijana kupitia mradi wa Kuijenga Kesho iliyo Bora (BBT) chini ya Wizara ya Kilimo ni kipimo cha matumizi mazuri ya mbolea.

Alieleza hayo tarehe 07 Agosti, 2023 alipokuwa akizungumza na vijana barani Afrika juu ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali mbalimbali katika kuhakikisha vijana wanaingia kwenye shughuli za uzalishaji na kupunguza changamoto ya ajira inayowakabili.

Aliongeza kuwa, ishara nyingine ni kuongezeka kwa mchango utokanao na kilimo kwenye uchumi wa nchi, kiasi cha mazao yanayopelekwa sokoni pamoja na kushuka kwa gharama za chakula sokoni.

Mjadala huu ni miongoni mwa mijadala mbalimbali iliyofanyika kuanzia tarehe 5 - 8 Agosti, 2023 wakati wa mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika ambapo zaidi ya washiriki 4000 kutoka nchi mbalimbali Afrika walishiriki mkutano huo.

Kwa upande wake Rais wa Kenya Mhe. Dkt. William Ruto akizungumza katika mkutano huo alisema pamoja na kuwekeza katika teknolojia za kilimo cha kisasa, matumizi sahihi ya mbolea na mbegu husaidia katika kuongeza kipato na kuleta mapinduzi ya kilimo barani Afrika.

Alisema nchi yake inawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwawezesha kupata mbolea na mbegu kwa bei himilivu, alieleza kuwa, nchi yake kwa mwaka 2023 imesajili wakulima 5000 na kusambaza mbolea kwa kutumia mtandao wa kielectroniki ili kuondoa madalali na matapeli ambao mara zote huwafanya wakulima kupata mbolea kwa gharama kubwa.

Alieleza kuwa, Kenya imepunguza gharama ya mbolea kutoka dola 50 hadi dola 20 kwa tani moja. Pamoja na hilo kupitia kampuni la mbolea la YARA Kenya imeongeza kiwango cha utoaji wa mbolea katika msimu uliopia na hivyo kutegemea kuvuna majunia milioni 44 hadi majunia milioni 61 ya mahindi kutokana na kutumia mbegu bora na kuhakikisha upatikanaji mzuri wa mbolea utakaochochea kupatikana kwa mazao mengi shambani.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Mawaziri wa wizara mbalimbali, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, Wakuu wa Mikoa na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kutoka ndani nan je ya nchi.


RESERVED









# Ruzuku ya mbolea ina ukomo: Rais Dkt. Samia



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipungia wananchi wa kusini wakati wa ziara yake ya kikazi katika mkoa wa Lindi katikati ya mwezi Septemba, 2023

Imeelezwa kuwa ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan si ya kudumu kwani kuna wakati mkulima atatakiwa kuinunua kwa bei halisi ya soko.

Wakulima wametakiwa kuweka akiba ya fedha wanayoipata kupitia mauzo ya mazao yao ili ziwasaidie kuendeleza shughuli za kilimo ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kumudu gharama ya mbolea pindi ruzuku itakapokoma.

Rais Mhe. Dkt. Samia alitoa kauli hiyo nyakati tofauti tarehe 18 Septemba alipokuwa akihutubia wananchi wakati wa ziara yake mkoani Lindi.

"Ni muhimu kuwa na matumizi mazuri ya fedha zinazotokana na kilimo ili muinuke kiuchumi na kuwa na uwezo wa kujitegemea kununua mbolea kwa kuwa misaada inayotolewa na serikali ina mwisho wake", Dkt. Samia amesisitiza.

Aidha, Rais Dkt. Samia alisema Serikali inafanya kazi kubwa kuwatengenezea mazingira rafiki ya kilimo ikiwa ni pamoja na kutoa ruzuku ya mbolea na kutafuta masoko ya mazao yatokanayo na kilimo lengo kuu ikiwa ni kuwainua kiuchumi na kueleza kuwa juhudi hizo zitagonga mwamba wasipokuwa na matumizi mazuri ya fedha wanazozipata.

Alisema, Serikali ipo katika mikakati ya kuboresha kilimo ikiwamo kupandisha thamani ya korosho, mbaazi na ufuta ili wakulima waweze kuuza kwa bei nzuri na kuwasisitiza wakulima hao kuongeza uzalishaji.

Mwisho Rais Dkt. Samia aliwataka kudumisha amani na utulivu ili kuwawezesha viongozi kufanyia kazi miradi ya maendeleo na kueleza uwepo wa uhasama na mapigano unawakosesha muda wa kufanya mambo ya maendeleo na badala yake wanajikita katika kutatua migogoro ya wananchi wake.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na viongozi waliofika kumpokea alipowasili kwa ziara ya kikazi katika mikoa ya kusini




Wananchi wa Mkoa wa Lindi wakipeperusha bendera ya Tanzania wakati wakimpokea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliowasiri mkoani humo kwa ziara ya kikazi






# Utegemezi wa mbolea nje ya Afrika wapelekea matumizi hafifu, uzalishaji mdogo

Imeelezwa kuwa, mbolea nyingi inayotumika Afrika inatoka nje ya bara hilo, wakati ile inayotengenezwa Afrika inauzwa nje ya bara hilo.

Hayo yalibainishwa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda akizungumza kando ya mkutano wa Mifumo ya Chakula Barani Afrika wakati wa majadiliano kuhusu ajenda ya mbolea Barani Afrika na afya ya udongo iliyofanyika katika ukumbi wa Selous ndani ya jengo la mikutano ya kimataifa la Julius K. Nyerere Jijini Dar Es Salaam tarehe 6 Agosti, 2023.

Waziri Mkuu mstaafu Pinda alisema, zaidi ya asilimia 90 ya mbolea nchini inaagizwa kutoka nje huku chini ya asilimia kumi ikitengenezwa ndani ya nchi.

Aliongeza kuwa, kwa sasa mbolea inayopatikana nchini inatoka nchi mbalimbali ikiwemo Russia, na kwa sasa upatikanaji wake umekuwa na changamoto kutokana na vita inayoendelea katika nchi hiyo.

Pinda aliongeza kuwa, hali hiyo imesababisha bei ya mbolea kupanda na pia mbolea kuadimika na kufikia kuhatarisha usalama wa chakula kwa baadhi ya nchi za Afrika.

Aliongeza kuwa, kutokana na bei ya mbolea kupanda duniani, Serikali za nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania zimeanzisha programu wezeshi za kusaidia upatikanaji wa mbolea ili kuleta suluhu ya changamoto hiyo kwa kuweka ruzuku kwenye pembejeo hiyo.

Kwa upande mwingine Pinda alisema matumizi ya mbolea yasiyofaa yamechangia kuendelea kuzorota kwa afya ya udongo na kusababisha mavuno kuwa hafifu.

Akizungumza alipokuwa akikaribisha mjadala kuhusu tasnia ya mbolea na afya ya udongo Rais wa Agra Afrika Dr. Agness Kalebata alisema asilimia hamsini (50%) ya chakula kinacholiwa duniani kinazalishwa kwa kutumia mbolea.

Akaongeza kuwa, matumizi ya mbolea yameendelea kuwa hafifu kutokana na upatikanaji wake kuwa mdogo na hivyo kupelekea uzalishaji mdogo wa mazao.

Akizungumza wakati wa majadiliano mmoja wa Pannelist alieleza kuwa, bara la Afrika linahitaji kuongeza uzalishaji wa mbolea ili kupunguza utegemezi kutoka nchi zilizoendelea na hivyo kutuhakikishia afya bora ya udongo unaotumika katika kuzalisha mazao.

Aliongeza kuwa, udongo unahitaji virutubisho kama vile mwili wa mwanadamu unavyohitaji ili uendelee kuzalisha na kuleta tija kwa wakulima.

Imeshauriwa serikali mbalimbali barani Afrika kufanya kazi bega kwa bega na taasisi binafsi ili kutatua changamoto ya pembejeo ya mbolea.

Kufanya kazi, kuboresha mbegu na kuhakikisha mbolea bora inapatikana kwa wakati sahihi na mahala sahihi kutawawezesha wakulima kuzalisha kwa tija na kuinua vipato vyao.











RESERVED

# Naibu Waziri Silinde aitaka TFRA kuimarisha Udhibiti wa Mbolea

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Ernest Silinde ametoa rai kwa Bodi ya wakurugeni na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuendelea kuongeza kasi ya udhibiti wa mbolea hususani katika maeneo ya mipakani ili mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali iwanufaishe watanzania na si kutoroshwa nje ya nchi.

Naibu Waziri Silinde ametoa rai hiyo leo tarehe 30 Septemba, 2023 alipotembelea na kuzungumza na uongozi wa Mamlaka hiyo katika ziara iliyolenga kujifunza namna Mamaka inavyofanya kazi na kutoa maelekezo ya Serikali katika kuimarisha utendaji kwa maslahi mapana ya taifa.

Amesema awali kilimo kilikuwa hakieleweki lakini kutokana na Serikali ya Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuamua kuweka nguvu kubwa katika kuinua Sekta ya Kilimo wakulima wameelewa na wameanza kufuatilia na kutokana na hilo changamoto mbalimbali zinaibuliwa kutoka huko chini.

Aidha, Mhe. Silinde ameitaka TFRA kuanza zoezi la usambazaji wa mbolea mapema ili kupunguza malalamiko ya kuwafikishia wakulima mbolea kwa kuchelewa kama ilivyojitokeza msimu uliopita wa kilimo.

Amesema mbolea zikipelekwa mapema itawawezesha wakulima kujiandaa mapema kwa kununua na kuhifadhi mbolea majumbani mwao wakisubiri msimu wa kupanda.

“kilichopo sasa kianze kusambazwa kisisubiri Wakai wa msimu ndipo tuanze kukimbizana kupeleka mbolea kwa wakulima” Mhe. Silinde alisisitiza.

Katika kuhakikisha ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali inawafikia walengwa, Naibu Waziri Silinde ameitaka TFRA kufanya uhakiki wa taarifa za usajili wa wakulima ilikuondoa changamoto za mawakala kuuza mbolea kwa wakulima waliotoa taarifa za uongo wakati wa usajili.

Ameipongeza Mamlaka kwa kuja na mfumo wa ramani unaoiwezesha kuoa maeneo walipo mawakala, kiasi cha mbolea walichonacho mawakala wa mbolea kwa nchi nzima na kueleza hiyo itasaidia kufuatilia upatikanaji wa mbolea kwa wakati katika maeneo yote

Naye mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku, Louis Kasera amesema utoajiwa mbolea ya ruzuku kwa wakulima kumeamsha hari ya wakulima wengi kutumia mbolea katika kilimo chao na hivyo uhitaji wa bidhaa hiyo kuwa mkubwa.

Amesema mamlaka imetatua changamoto ya usambazaji iliyojitokeza msimu uliopita wa kilimo kwa kusajili vyama va ushirika 198 nchi nzima na Vyama vidogo vya ushirika (AMCOSS) zaidi ya 2000 vitakavyosaidia kufikisha mbolea kwa wakulima wao hata katika maeneo ya pembezoni.

Amesema, lengo la Mamlaka mkulima asitembee Zaidi ya umbali wa kilomita 15 kwenda kutafuta mbolea na hivyo wamepanga bei elekezi kulingana nae neo ambalo mbolea inafika.

Katika kuongeza Udhibiti wa kuuza mbolea mara mbili, Louis amesema Mamlaka imeboresha mfumo ambapo kila mfuko wa mbolea utakaouzwa namba ya siri itakayokuwa imetumika haitatumika ten ana mkulima atapokea namba nyingine itakayomruhusu kununua mbolea kulingana na ukubwa wa shamba alioandikisha wakati wa usajili.

Akitoa neno la shukrani Mkurugenzi wa Huduma za mamlaka (DCS), Victoria Elangwa alishukuru uamuzi wa Naibu Waziri Silinde kutembelea Mamlaka na kueleza ujio wake utachochea hari ya kufanya kazi kwa menejimenti na watumishi wa Mamlaka.



Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde akizungumza jambo wakati wa kikao baina yake na uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na wajumbe wa kamati ya ruzuku kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 30Septemba, 2023. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo Dkt. Anthony Diallo



Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo Dkt. Anthony Diallo wakiwa katika kikao na Menejimenti na wajumbe wa kamati ya ruzuku kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 30 Septemba, 2023.






Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti na wajumbe wa kamati ya ruzuku kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehe 30 Septemba, 2023. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo Dkt. Anthony Diallo

# TFRA yampokea Mkurugenzi Mteule Joel Laurent

Mkurugenzi Mtendaji Mteule wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent leo tarehe 2 Oktoba, 2023, amewasili zilipo ofisi za Mamlaka na kuwa na mazungumzo mafupi na aliyekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Dkt. Stephen Ngailo, Menejimenti na Kamati ya Ruzuku ya mbolea ya TFRA.

Akizungumza katika kikao kilichofanyika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka Bw. Laurent ameshukuru kwa mapokezi mazuri na kuahidi kuendelea kutekeleza majukumu ya mamlaka kuanzia pale mtangulizi wake alipoishia.

“Nimefurahi kuona nyuso za furaha na nimejihisi nipo sehemu sahihi kabisa” Bw. Laurent aliongeza.

Pamoja na hayo, mkurugenzi Laurent katika kikao baina yake na watumishi wote wa mamlaka cha tarehe 6 Oktoba, 2023, aliwataka watumishi wa Mamlaka kuhakikisha wanaijua na kusimamia ipasavyo ruzuku ya mbolea na kueleza hilo ni jukumu la watumishi wote.

“kila mtumishi ahusike katika kuijua, kuiboresha na katika kuifanyia kazi ruzuku. Hapo kwenye kuifanyia kazi ndio pa muhimu sana sawa watumishi?” Laurent alisisitiza.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Dkt. Ngailo ametoa shukrani kwa menejimenti na watumishi wote wa TFRA kwa ushirikiano waliompa wakati wote wa utumishi wake katika ofisi hiyo na kueleza kuwa aliishi kwa amani.

Amewaasa menejimenti na watumishi kumpa ushirikiano wa kutosha Mkurugenzi mpya na kueleza kufanikiwa kwa mkurugenzi Laurent ni mafanikio ya taasisi kwa ujumla wake.

“Be honest kwake, mkimshauri kwa nia njema akifanikiwa yeye taasisi imefanikiwa na si kumpa ushauri ili aanguke” Dkt. Ngailo amesisitiza.

Amesema wakati wake kutumika hapo umekwisha lakini atakuwa tayari atakapohitajika ili kutoa ushauri wakati wowote hivyo wasisite kumtafuta.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa TFRA, Mkurugenzi Mteule Laurent alikuwa akifundisha katika chuo cha sheria (school of Law) Jijini Dar es Salaam, lakini pia amefundisha vyuo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mzumbe, SUA, Tumaini na kutumika katika maeneo mbalimbali mahala kwingineko.



Mkurugenzi Mtendaji Mteule wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili ofisini kwake Jijini Dar Es Salaam anayeshuhudia ni aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo Dkt. Stephan Ngailo tarehe 02 Oktoba, 2023.



Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Bi. Victoria Elangwa (wa pili kushoto) akimkaribisha Mkurugenzi Mtendaji Mteule wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent (kushoto) mara baada ya kuwasili zilipo ofisi za Mamlaka tarehe 2 Oktoba, 2023.

# HABARI KATIKA PICHA





Mkurugenzi Mtendaji Mteule wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent akisalimiana na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja Bw. Joseph Charos alipowasili ofisini hapo mara baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo mwishoni mwa wiki.



Watumishi wa Mamlaka wakifuatilia maelezo yaliyokuwa yakitolewa na Mkurugenzi Mpya wa Mamlaka hiyo (hayupo pichani) katika kikao kifupi kilichofanyika katia viwanja vya Mamlaka jijini Dar es Salaam tarehe 6 Oktoba, 2023.





Mkurugenzi Mtendaji Mteule wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bw. Joel Laurent (kulia) akimsikiliza aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo Dkt. Stephan Ngailo (kushoto) wakati wa kikao kifupi baina yao, Menejimenti ya TFRA na wajumbe wa kamati ya ruzuku ya Mamlaka (hawapo pichani) alipokwenda kwa ajili ya kuripoti mara baada ya kuteuliwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hiyo hivi karibuni.



# TFRA yapongezwa upatikanaji wa mbolea kabla ya msimu



Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TFRA wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mhandisi Juma Omary Mdeke (mwenye miwani) na Katibu wake, Victoria Elangwa (kulia) wakibadilishana mawazo mara baada ya kufunga kikao kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka tarehee 12 Septemba, 2023 Jijini Dar Es Salaam.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Patrick Mwalunenge ameipongeza TFRA kwa kuhakikisha mbolea zinapatikana katika maeneo mengi nchini na kuwawezesha wakulima kufanya maandalizi kwa kununua mbolea hizo mapema.

"Nimezunguka maeneo mengi, mbolea ipo na wakulima wananunua na kuhifadhi hivyo niwapongeze sana kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya" Alisema Mwalunenge.

Mwalunenge ametoa pongezi hizo leo mara baada ya kumaliza kikao cha kamati ya Bodi ya Fedha, Mipango na Utawala kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka Jijini Dar es Salaam.

Akihitimisha kikao hicho, mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Mipango na Utawala, Mhandisi Juma Omary Mdeke amewashukuru wajumbe wa kamati na menejimenti ya TFRA kwa kushiriki kikamilifu katika kujadili mada mbalimbali na kupokea maoni yaliyotolewa ili kuboresha utendaji na hivyo kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwenye tasnia ya mbolea.

Aidha, Mhandisi Mdeke ameitaka Menejimenti kuishirikisha bodi hiyo mambo inayokutana nayo ili kwa pamoja waone namna bora ya kuboresha tasnia hiyo na hivyo kufikia maono ya kitaifa katika kuwahudumia wakulima.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo amewashukuru wajumbe wa bodi na menejiment kwa ujumla kwa mawazo chanya yatakayosaidia kuboresha tasnia katika majukumu yake ya kila siku.

Kikao hicho cha siku moja ni maandalizi kuelekea kikao cha Bodi kinachotarajia kufanyika hivi karibuni ikiwa ni kwa mujibu wa miongozo na taratibu za usimamizi wa Mamlaka za Serikali.









# WAKULIMA WAHAMASISHWA KUTUMIA MBOLEA MOMBA

Wakulima halmashauri ya Momba tarafa ya Msangano na Kamsamba wametakiwa kuondokana na dhana potofu kwamba kutumia mbolea kunaharibu udongo kwani kwa kufanya hivyo ni kujichelewesha wenyewe kupata mafanikio na kuinua uchumi wao.

Hayo yalisemwa na wataalamu wa masuala ya mbolea kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Bw. Henerico Renatus na Daniel Maarifa wakati wa semina zinazoendelea kwa wakulima katika halmashauri ya Momba na timu ya wataalamu kutoka wizara ya kilimo na ushirika waliokita kambi ya siku 14 kutoa elimu ya kilimo bora na chenye tija kwa kwa wakuliama.

"Haya mawazo tunaomba wakulima wa huku bondeni muachene nayo kabisa kwani yanawachelewesha kufikia mafanikio, kwa karne hii huwezi kukwepa matumizi ya mbolea, kwanza ardhi imechoka inahitaji kuiongezea rutuba kupitia mbolea" Henerico alisistiza.

Kwaupande wake mratibu wa utafiti na ubinifu kutoka taasisi ya utafiti wa kilimo Tanzania Tari-Ilonga Meshack Makenge, alisema mafanikio mengine katika kilimo ni wakulima kuzingatia uchaguzi sahihi wa mbegu na kupanda kwa kufuata ushauri wa kitaalam.

"Tunapozungumzia kilimo biashara na chenye kuleta tija matumizi ya mbegu bora ni jambo la msingi sana, matumizi ya mbegu za asili zinakufanya wewe mkulima kutumia nguvu kubwa kwa kulima shamba kubwa lakini mavuno kidogo" Makenge aliongeza.

Mratibu wa uhaulishaji wa teknolojia na mahusiano Tari-Ilonga, Lilian Mwanga alisema katika kuwasaidia wakulima Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inazo teknolojia mbalimbali za kisasa zinazomwezesha mkulima kufikia mafanikio ya haraka kupitia sekta ya kilimo.

"Tunapozungumzia teknolojia ni pamoja na mbegu bora za mazao mbalimbali, ikiwemo mahindi, alizeti, mtama, ufuta na mazoa yote ya mikunde ambayo, kwa asilimia kubwa tasisi yetu ya Tari inazalisha" Mwanga

Rosemary Simchimba na Daud Mtaturu ni wakulima wa kijiji cha Momba, walisema changamoto inayosababisha wakulima wa Momba ukanda wa chini kutotumia mbolea walikosa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea hizo na hata hivyo mbolea hizo hazifiki kwa wakati na hata upatikanaji wake ni mgumu.

"Walikuja wataalamu hapa kijijini kwetu wakatuandikisha na kuchukua majina yetu kwa ajili ya mbolea, lakini cha kushangaza awamu zote mbili hawakutuletea mbolea na ndiyo maana tulikata tamaa na kuendelea kulima kama tulivyo zoea miaka yote" Simchimba alieleza.

Akijibu hoja hiyo Bw. Henerico alisema Jambo hilo halitajitokeza tena na kuahidi kutoa mafunzo kwa watu wote wanaotaka kuanzisha biashara ya Mbolea katika Halmashauri ya Momba siku ya tarehe 9-10 mwezi Oktoba, 2023 na kuwaunganisha na Kampuni la Mbolea la Taifa (TFC) ili mbolea zipatikane ngazi ya kata muda wote.

Kwaupande wake Mbunge wa Jimbo la Momba Mheshimiwa Condester Sichalwe, alisema kipindi hiki ambacho yeye ndiye mbunge anatamani kuona watu wake wanakomboka na kilimo cha utumwa kisichokuwa na manufaa.



Mbunge wa Momba Mkoa wa Songwe, Condester Michael Sichalwe akizungumza nawananchi wa Momba wakati wa mafunzo yaliyoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)



Wananchi wa Momba wakifuatilia mada wakati wa mafunzo na uhamasishaji wa wakulima kujiandikisha ili kunufaika na mbolea za ruzuku uliofanyika Momba Mkoani Songwe






Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Henerico Renatus akitoa mada kwa wakulima wa Momba mkoani Songwe alipofika kutoa elimu ya mbolea kwa wakulima hao

# Wafanyabiashara 71 Arusha wajengewa uwezo




Wahitimu 71 wa mafunzo ya mbolea Kanda ya Kaskazini wakionesha vyeti vyao baada ya mafunzo kuhitimishwa. Wasio na vyeti ni Maafisa Udhibiti Ubora wa TFRA Kanda walioratibu na kuyoa mafunzo hayo

Wafanyabiashara 71 wapatiwa mafunzo ya matumizi sahihi ya Mbolea yaliyofanyika Mkoani Arusha na kumalizika tarehe 22-09-2023.

Mafunzo yamefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Cedha ulipo jijini Arusha ambapo jumla ya wafanyabiashara wa mbolea 71 walipewa mafunzo hayo na kutunukiwa vyeti vya mafunzo.

Washiriki hao wameishukuru Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya kaskazini kwa kuratibu na kuwezesha mafunzo hayo yaliyoonesha kufanikiwa kwa sehemu kubwa.



Wadau wakifuatilia mafunzo kutoka kwa Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA Kanda ya Kaskazini, Bi Lydia Kalala hivi karibuni



# Watumishi 26 TFRA wajengewa uwezo masuala ya Vipimo

Watumishi wa Idara ya Huduma za Udhibiti wakiongozwa na Mkurugenzi wake, Bi. Happiness Mbelle wameshiriki mafunzo ya vipimo yaliyowajengea uwezo wa kutambua dhana ujazo hivyo kuwasaidia kusimamia kikamilifu jukumu la udhibiti wa mbolea.

Mafunzo hayo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) yalitolewa kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 20 Septemba, 2023 katika ukumbi wa KCC Kibaha mkoani Pwani, yakiwa na jumla ya washiriki 26 kutoka TFRA.

Pamoja na watumishi kutoka Makao makuu ya TFRA, Meneja na maafisa Udhibiti Ubora kutoka ofisi za kanda walishiriki mafunzo hayo.





# HABARI KATIKA PICHA









Tanzania Fertilizer Regulatory Authority

AGRF 2023




Mhe. Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika Mjadala wa masuala ya Kilimo na Vijana wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika **(AGRF 2023)** unaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC)

## Hongera

**Bw. Joel Laurent**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wote wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) inakupongeza kwa kuteuliwa na Mhe Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka. Tunakuahidi ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yako.

**Karibu TFRA**



"MBOLEA BORA KWA WAKULIMA WOTE"

## Shukrani

**Dkt. Stephan Ngailo**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wote wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) tunakushukuru kwa ushirikiano uliotupa ulipokuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA. Tunakutakia majukumu mema.

"MBOLEA BORA KWA WAKULIMA WOTE"



@tfra_Official   Tanzania Fertilizer Regulatory Authority   AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA

Tanzania Fertilizer Regulatory Authority

AGRF 2023



> The key objectives of the Tanzania Government towards food systems transformation initiatives is cognizance of the challenges emanating from Climate change, by including regenerative production systems (Soil health technologies, use of less on-farm inputs like agrochemicals and fertilizers), while promoting judicious use of off-farm inputs.

*DKT. PHILIP ISDOR MPANGO - Vice President United Republic of Tanzania*

## PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na watumishi wote wa TFRA tunakupongeza kwa kuteuliwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Madini.

Tunashukuru kwa ushirikiano wako ulipokuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo. Tunakutakia utumishi mwema



AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA

MHE. ANTHONY MAVUNDE (Mb)

## PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na watumishi wote wa TFRA tunakupongeza kwa kuteuliwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Naibu Waziri wa Kilimo.

Tunakuahidi ushirikiano wakati wote ukihudumu katika nafasi hiyo.



AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA

MHE. DAVID SILINDE (Mb)

@tfra_Official  Tanzania Fertilizer Regulatory Authority

AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA












Pamoja na kuimarisha afya na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza, watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ( TFRA) wakiongozwa na Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe wametoa elimu ya mbolea kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga.

Washiriki hao wametoa elimu hiyo waliposhiriki mbio zilizofanyika mkoani Tanga tarehe 17 Septemba, 2023.